

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dar es Salaam
26 Julai, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewataka Viongozi kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Ibara ya 8 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayowataka kuwathamini na kuwaheshimu wananchi.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo leo Ikulu, wakati akiwaapisha Viongozi mbalimbali wakiwemo Mawaziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Makatibu Tawala wa Mikoa pamoja na Balozi.

Aidha, Rais Dkt. Samia amewataka viongozi hao kusimamia viapo walivyoapa mbele ya Mamlaka iliyowateua na mbele ya wananchi wanaokwenda kuwatumikia kwa kuhakikisha maslahi ya wananchi yanalindwa.

Kwa upande mwingine, Rais Dkt. Samia amemuagiza Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Jerry Silaa kuendelea kusimamia kikamilifu uhuru wa habari kwa kushirikiana na wadau wa sekta hiyo.

Rais Dkt. Samia pia amemtaka Waziri huyo kusimamia kasi ya ujenzi wa minara ya mawasiliano simu vijijini na kuimarisha usikivu wa redio ya Taifa kwenye maeneo ya pembezoni.

Vile vile, Rais Dkt. Samia amemtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhe. Ridhiwani Kikwete kuhakikisha vijana wanapata ajira kupitia Wizara za kisekta kama vile kilimo, mifugo, uvuvi na madini.

Hali kadhalika, Rais Dkt. Samia amemtaka Waziri huyo kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kuhakikisha inaendeshwa kisayansi, inakuwa endelevu pamoja na kusimamia miradi inayotekelezwa na mifuko hiyo.

Kwa upande wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Rais Dkt. Samia amemtaka Mhe. Balozi Mahmoud Thabit Kombo kuboresha utendaji na kulinda heshima ya nchi kimataifa.

A handwritten signature in blue ink, appearing to be 'Sharifa B. Nyanga'.

Sharifa B. Nyanga
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

